Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 3 Issue 1 | [December] [2026] | [Page 124] – [Page 149]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

Mchango wa Rais Sheikh Abeid Amani Karume, Katika Maendeleo ya Kiswahili: Uchambuzi wa Sera, Matamko na Mipango

Sauda Uba Juma, Ahmad Yahya Sovu, Editha Adolph, Majura Nyangaywa Lugembe, Njana Masanja
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

Corresponding author: chudam017@gmail.com

Article History:
Received: May 31, 2026
Accepted: July 20, 2026
Published: Oct 27 2026

Maneno Muhimu:
mchango, lugha ya Kiswahili, sera ya lugha, matamko ya lugha, mipango ya lugha, Rais Abeid Amani Karume

This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license

Ikisiri

Historia inaeleza kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizotawaliwa na wageni kwa muda mrefu. Katika utawala huo, lugha ya Kiswahili ilikebehiwa na kutwezwa hivyo kutotumika katika maeneo rasmi (BAKIZA, 2020). Lugha za Kiingereza na Kiarabu ndizo zilizopewa hadhi ya juu katika shughuli za kiserikali. Hata hivyo, mara baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, inasemekana kuwa lugha ya Kiswahili ilihuishwa upya na kupatiwa nafasi maalumu chini ya uongozi wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Mheshimiwa Sheikh Abeid Amani Karume. Pamoja na dai hilo kurudiwa mara kwa mara katika machapisho mbalimbali, halijawahi kuchunguzwa kwa kina kwa kubainisha rasmi ni sera zipi, matamko yapi na mipango ipi hasa iliyowekwa na serikali yake. Hivyo, makala hii inalenga kuchunguza mchango wa Rais Karume katika kuweka msingi wa maendeleo ya Kiswahili Zanzibar enzi za uongozi wake (1964-1972), kwa kubainisha na kuchambua kwa utaratibu sera, matamko na mipango aliyoiweka. Utafiti huu ni matokeo ya data zilizokusanywa kutoka maktabani na pia nyanjani. Mbinu za usaili na hojaji ndizo zilizotumika katika utafiti huu, na data zimechanganuliwa kwa kutumia

mkabala wa kitaamuli. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Sera na Mipango ya Lugha iliyoasisiwa na Haugen mwaka (1966). Kwa ujumla, matokeo ya uchunguzi yamedhihirisha kwamba Rais Abeid Amani Karume aliweka misingi imara katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili Zanzibar: kwa upande wa sera, alikitangaza kuwa lugha rasmi ya ofisi, elimu na vyombo vya habari; kwa upande wa matamko, aliyageuza mahutubio yake kuwa chombo cha kujenga utaifa na uzalendo kupitia Kiswahili; na kwa upande wa mipango, alisimamia utekelezaji thabiti kupitia kampeni ya kufuta ujinga, mitihani ya walimu, uundaji wa istilahi mpya na ubadilishaji wa majina ya maeneo. Hivyo, makala inapendekeza viongozi wengine kusisitiza matumizi bora ya Kiswahili katika jamii na kuenzi mchango huo wa viongozi waandamizi na waasisi kwa vitendo. Aidha, inapendekezwa tafiti zaidi zifanyike kubaini michango ya viongozi wengine wa Zanzibar waliofuata pamoja na viongozi wa nchi nyingine kwa ujumla.

1.0 Utangulizi

Mnamo miaka 1832-1964 Zanzibar ilikuwa chini ya tawala za wageni kutoka nje ya Afrika. Watawala maarufu walikuwa Waarabu na Waingereza. Kipindi cha utawala wa Waarabu wa Oman lugha ya Kiarabu ilikuwa lugha ya serikali, dini na tabaka tawala, ilikuwa lugha ya Sultani mahakamani na nyaraka rasmi. Mtu yeyote aliyetaka kuwa karibu na madaraka alilazimika kujifunza Kiarabu (Mazrui na Mazrui, 1995). Aidha, lugha ya Kiarabu ilikuwa ikitumiwa katika kufundishia madrasa za Qur'ani na elimu ya dini. Ingawa lugha ya Kiswahili haikupigwa marufuku, lakini ilichukuliwa kama lugha ya watu wa chini wakiwamo

wafanyabiashara wadogo, watumwa na wenyeji wa Pwani. Hata hivyo, juhudi hizo hazikufua dafu kwa kuwa lugha ya Kiarabu haikupata nafasi ya kuwa lugha ya mawasiliano ya watu katika jamii. Pamoja na hali hiyo, lugha ya Kiarabu iliacha alama kubwa kwenye lugha ya Kiswahili na utamaduni wa Zanzibar kwa ujumla. Hali hiyo ilichanuzwa kwa kuwa Waarabu walitamalaki Zanzibar kwa muda mrefu na hivyo basi, kupenyeza msamiati mwingi katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Waingereza walitawala Zanzibar mnamo mwaka 1890-1963. Katika kipindi cha utawala wao, Kiswahili kilipanda hadhi kikilinganishwa na kipindi cha utawala wa Waarabu. Kwa mujibu wa Shariff (1991) Waingereza walianza kukitumia Kiswahili katika mawasiliano ya mikoa pamoja na mahakama za chini. Aidha, Kiswahili kilipata nafasi ya kuingizwa katika mfumo wa elimu (BAKIZA, 2020). Waingereza walianzisha shule za serikali ambapo Kiswahili kilianza kufundishwa kama somo na pia kilitumika kufundishia masomo mengine katika ngazi ya msingi. Sanjari na hatua hiyo, Waingereza walikitumia Kiswahili katika mawasiliano yao na wenyeji. Pia, walibadilisha uandishi kutoka herufi za Kiarabu kwenda herufi za kilatini ili uchapishaji uwe rahisi. Hivyo, mnamo mwaka 1930 utawala wa Waingereza ulipendekeza kuundwa kwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki, (Inter-Territorial Language Swahili Committee) ambayo ilipewa jukumu la kusimamia suala zima la usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Mchakato wa usanifishaji ulihusu uchaguzi wa lahaja moja ambayo itatumika kama msingi wa usanifishaji. Hivyo Kamati hiyo, iliiteua lahaja ya Kiunguja mjini kuwa msingi wa usanifishaji huo. Bila shaka Kiunguja mjini hakikuteuliwa kwa bahati mbaya, bali lahaja hiyo iliteuliwa kutokana na sababu za msingi zilizoonekana kuwa ilifaa kusanifishwa. Mbaabu (2007), anaeleza kwamba kabla ya Kiunguja kuteuliwa kuwa lahaja ya usanifishaji, lahaja hiyo ilipata upinzani mkubwa dhidi ya lahaja ya Mombasa, Lamu na Patte ambazo zilipendekezwa na kuonekana zingefaa zaidi ya

Kiunguja. Hata hivyo, Kiunguja mjini kilionekana kuwa na umuhimu wake zaidi endapo kitasanifishwa. Kwa mnasaba huo, Kiswahili sanifu kinachotumika hii leo kilichipukia Zanzibar.

Muktadha huu wa kihistoria unaonesha kwamba, kabla ya Mapinduzi ya 1964, hadhi ya Kiswahili Zanzibar ilikuwa imejengwa hatua kwa hatua na tawala za kigeni, bila hata mara moja Kiswahili kupewa mamlaka kamili ya lugha ya taifa au ya utawala. Ni katika muktadha huu wa kihistoria ndipo mchango wa Rais Abeid Amani Karume unapopata umuhimu wake wa pekee: badala ya kuendeleza mfumo alioukuta, Rais Karume alichagua kuupindua kwa kuipa Kiswahili mamlaka kamili ya kisiasa, kiutawala na kijamii. Vivyo hivyo, uzoefu wa Zanzibar hauko peke yake; nchi nyingine za Afrika zilizopata uhuru kipindi hicho, kama Tanzania Bara chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Kenya na Uganda, nazo zilikabiliwa na uamuzi kama huo wa kuchagua lugha ipi iwe chombo cha umoja wa kitaifa baada ya ukoloni. Mazrui na Mazrui (1995) wanaeleza kwa kina jinsi uaamuzi huo wa kisiasa ulivyoathiri hatima ya Kiswahili katika eneo zima la Afrika Mashariki. Hata hivyo, tofauti na baadhi ya nchi jirani zilizoendelea kutumia lugha za kikoloni sanjari na lugha za kienyeji, Zanzibar chini ya Rais Karume ilichukua msimamo mkali zaidi wa kuachana kabisa na Kiingereza katika nyanja rasmi, jambo linalostahili kuchunguzwa kwa kina zaidi.

Mapitio ya Maandiko Yaliyotangulia na Pengo la Kiutafiti

Tafiti kadhaa zimejadili historia ya sera za lugha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Mazrui na Mazrui (1995) wanaeleza kwa mapana jinsi Kiswahili kilivyopanda hadhi kisiasa na kiuchumi barani Afrika Mashariki, wakigusia jukumu la viongozi wa kisiasa katika mchakato huo, lakini bila kujikita katika uchambuzi wa kina wa mtu mmoja mmoja miongoni mwa viongozi hao. Mbughuni (1974) kwa upande wake

anachambua sera ya kitamaduni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla, akinukuu baadhi ya hotuba za viongozi wakiwamo Karume, lakini lengo lake kuu ni sera ya kitaifa ya Muungano na sio uchambuzi mahususi wa Zanzibar peke yake. Shariff (1991) anaeleza kwa kina hali ya lugha na jamii ya Zanzibar wakati wa ukoloni, akitoa msingi mzuri wa kuelewa hali ya Kiswahili kabla ya Mapinduzi, lakini kazi yake haihusishi kipindi cha baada ya Mapinduzi. BAKIZA (2020) inaripoti maendeleo ya Kiswahili Zanzibar kati ya miaka 2010 hadi 2020, kipindi kilicho mbali sana na enzi za Rais Karume. Vilevile, Tibategeza na du Plessis (2018) wanachunguza nafasi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika sera ya elimu ya Tanzania kwa ujumla, wakigusia kwa ufupi tu mabadiliko ya mwaka 1967 bila kuyahusisha moja kwa moja na mtu aliyeyaanzisha. Ijapokuwa kazi hizi zote zimechangia pakubwa kuelewa mazingira mapana ya sera za lugha katika ukanda huu, hakuna hata moja iliyojikita rasmi katika kutenganisha na kuchambua kwa kina sera, matamko na mipango mahususi iliyowekwa na Rais Abeid Amani Karume mwenyewe kama mtu binafsi mwenye mamlaka. Pengo hili la kiutafiti ndilo linaloifanya makala hii kuwa muhimu, kwani inachunguza kwa undani jinsi Rais Karume, kama mtu mmoja mwenye dhamana ya uongozi, alivyotumia mamlaka yake kubuni sera, kutoa matamko na kusimamia mipango iliyoweka msingi wa maendeleo ya Kiswahili Zanzibar, jambo ambalo hadi sasa halijafanyiwa uchambuzi wa kina wa aina hii.

Makala hii inabainisha mchango wa Rais Abeid Aman Karume katika kuweka msingi wa maendeleo ya Kiswahili Zanzibar, kwa kuchambua bayana sera, matamko na mipango aliyoiweka enzi za uongozi wake. Hivyo, kwa kuwa mchango unaobainishwa katika utafiti huu unahusishwa moja kwa moja na mtu wa Rais Abeid Aman Karume mwenyewe, bila shaka litakuwa jambo jema tukigusia historia ya maisha yake walau kwa ufupi kabla ya kuingia katika uchambuzi wa

mchango wake.

1.1 Historia Fupi ya Hayati Abeid Amani Karume

Mzee Abeid Aman Karume alikuwa rais wa kwanza wa Zanzibar mara baada ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964. Aliingia madarakani katika awamu yake ya kwanza kuanzia (1964-1972). Katika kipindi cha kumbukizi ya Rais Abeid Amani Karume tarehe 6/4/2026, Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC-Zanzibar Broadcasting Corporation) na Wizara ya Elimu Zanzibar (1988) inaeleza kwamba Rais Karume alizaliwa Agosti 4, 1905 katika kitongoji cha Pongwe huko Mwera Wilaya ya Magharibi A, Unguja. Rais Abeid Karume ni mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia ya watoto watano (5) ya Amani Karume na Amina bint Kadir (Amina Kadudu). Alikuwa ni miongoni mwa watoto watatu wa kiume; watoto wawili wa kike walifariki kabla ya Rais Karume kuuawa hapo mwaka 1972. Alipata elimu ya msingi katika skuli ya msingi Mwera mwaka 1910, akasoma kwa muda wa miaka mitatu tu hadi 1913. Baadaye alihamia kwa babake mdogo mjini Unguja, ambaye alikuwa Sajenti wa jeshi la polisi la Sultani wa Zanzibar wakati huo. Aidha, akiwa na umri wa miaka 15, Rais Karume alianza kazi ya ubaharia kwenye boti ya mzigo kuanzia 1920-1938.

Rais Abeid Karume hakubahatika kwenda shule ya sekondari. Elimu yake aliipata kwa kusafiri, kufanya kazi na kujifunza kutoka katika mikutano na wasomi wa Kiafrika kama Kamuzu Banda alipokuwa Uingereza. Karume anatajwa kuwa, kupitia kazi yake ya ubaharia, alizidi kupata mawasiliano na watu wengi wa tabaka mbalimbali, kujifunza hali halisi ya maisha ya wafanyakazi na kufahamu changamoto kama uonevu, ajira na mazingira ya kazi. Uzoefu huu wa moja kwa moja na maisha ya wananchi wa kawaida ndio unaotoa mwanga wa kufahamu kwa nini, baadaye alipopanda madarakani, alichagua kuinua lugha ya wananchi hao wa

kawaida Kiswahili badala ya kuendelea kutegemea lugha za kigeni zilizokuwa zikitumiwa na tabaka tawala pekee. Rais Abeid Karume alirudi Zanzibar miaka ya 1940-1950 ambapo alikuta hali ngumu ya uchumi kwa wananchi wa Zanzibar. Asilimia 13 ya Waarabu walimiliki asilimia 80 ya ardhi nzuri, Waafrika wengi walikuwa vibarua mashambani katika ardhi yao na walitengwa kisiasa chini ya utawala wa Kisultani na Waingereza. Hapo ndipo akaanza kuhamasisha watu wa kawaida kupinga udhalimu huo.

Safari yake ya kisiasa, kwa mujibu wa The Citizen (2025), ilianza yeye na wenzake walipounganisha vyama vidogo vidogo vya Waafrika na Shirazi na kuunda Afro Shirazi Party (ASP) mwaka 1957. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kupigania haki za Waafrika na Shirazi ambao walikuwa wengi lakini hawakuwa na sauti serikalini. Rais Abeid Karume alikuwa ndiye kiongozi mkuu kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuhutubia na kuwavuta watu aliokuwa nao. Kuelekea Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1961-1963, ASP ilishindwa kwenye chaguzi zilizopangwa na Waingereza ambapo vyama vya Waarabu vilishinda. Ilipofika Disemba mwaka 1963, Zanzibar ilipata uhuru kutoka kwa Waingereza lakini madaraka yakabaki kwa Sultani na Waarabu wachache. Baadaye, Januari 12, 1964 Rais Karume aliongoza Mapinduzi ya Zanzibar yaliyompindua Sultani Jamshid. Baada ya Mapinduzi hayo, Rais Abeid Karume aliiongoza Zanzibar kwa kipindi cha miaka minane tu, kwani mnamo tarehe 7 Aprili 1972, aliuawa kwa kupigwa risasi akiwa kwenye mkutano na viongozi wa chama Makao Makuu ya Afro Shirazi Party (ASP) Kisiwandui katika Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. Tukio hili ni moja kati ya matukio muhimu ya kihistoria yaliyowahi kutokea ndani ya Zanzibar.

2.0 Mwega wa Kinadharia

Data za makala hii zimechambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Sera na Mipango ya Lugha (Language Policy and Planning Theory). Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu Haugen mwaka (1966) katika kitabu chake Language Conflict and Language Policy: The Case of Modern Norwegian. Haugen alitumia dhana hii kuchambua jinsi Norway ilivyojenga na kupanga lugha yao ya kitaifa baada ya uhuru, hasa katika mazingira ambapo taifa jipya lilihitaji kuchagua na kuiendeleza lugha itakayowaunganisha wananchi wake baada ya vipindi virefu vya kutawaliwa. Nadharia hii inashughulikia uamuzi wa makusudi unaofanywa na serikali, taasisi au watu wenye mamlaka kuhusu lugha yao katika jamii. Misingi ya Nadharia ya Sera na Mipango ya Lugha inajengwa kwenye wazo kwamba lugha haijibadilishi yenyewe bali inabadilika kwa makusudio ya watu wenye mamlaka. Kwa ujumla, nadharia hii imejiegemeza kwenye misingi mitatu ifuatayo.

Mosi, mipango ya hadhi ya lugha (status planning), ambapo kiongozi yeyote mwenye mamlaka anaweza kuamua na kupangilia matumizi ya lugha katika nchi yake. Mathalani, kuchagua lugha gani iwe ya taifa, lugha rasmi au lugha ya mawasiliano ya kawaida katika jamii. Huu ndio mhimili unaohusu uamuzi wa kisera na kimamlaka kuhusu nafasi ya lugha katika jamii. Pili, mipango ya kongoo ya lugha (corpus planning), yenye maana kwamba kiongozi yeyote mwenye mamlaka anapaswa kubadilisha lugha yenyewe ili iendane na mahitaji ya jamii yake. Msingi huu unahakikisha kwamba lugha iliyoteuliwa inakuzwa kwa njia moja au nyingine ili isibaki tuli, kwa mfano kuiundia istilahi, kuandika vitabu na kamusi zenye ufafanuzi mbalimbali wa lugha husika, au hata kubadilisha majina ya maeneo ili yaendane na lugha mpya iliyopewa hadhi. Tatu, mipango ya upataji lugha (acquisition planning), ambapo kiongozi mwenye mamlaka vilevile anao wajibu wa kuhakikisha watu katika jamii yake wanapata fursa ya kujifunza lugha hiyo. Jambo hili linatekelezwa kupitia mitaala ya shule, vyombo vya habari na

mafunzo ya watu wazima.

Mihimili ya nadharia hii imekuwa faafu katika utafiti huu kwa sababu mchango wa Rais Karume katika kuweka msingi wa Kiswahili Zanzibar haukuwa wa kiisimu pekee bali ulikuwa wa kisiasa na kiutawala. Kuanzia mwaka 1964, serikali ya Mapinduzi chini ya Rais Abeid Aman Karume ilipitisha sera mbalimbali zilizolenga kuweka msingi madhubuti wa lugha ya Kiswahili. Hivyo, Kiswahili kilipata nafasi ya kuwa lugha ya serikali, elimu na mawasiliano ya umma. Kwa mnasaba huo, makala hii imechambua jinsi uamuzi huo ulivyosaidia kuweka msingi thabiti wa Kiswahili Zanzibar katika nyanja mbalimbali. Kwa msingi wa mihimili hiyo mitatu, uwasilishaji wa matokeo ya mchango wa Rais Karume umepangwa katika mafungu matatu bayana: Sera za Kiswahili (zinazowakilisha mipango ya hadhi ya lugha), Matamko ya Kiswahili (yanayoonesha jinsi hadhi hiyo ilivyotangazwa na kuenezwa kwa jamii kwa lugha ya kihisia na kiuzalendo), na Mipango ya Kiswahili (inayowakilisha mipango ya kongoo ya lugha na upataji lugha). Mpangilio huu unarahisisha kuonesha kwa uwazi jinsi mchango mmoja wa kiongozi mmoja Rais Karume ulivyogusa mihimili yote mitatu ya nadharia kwa wakati mmoja.

3.0 Methodolojia

Utafiti uliozaa makala hii ulikuwa wa kimaelezo na sio wa kitakwimu, kwa kuwa mwegamo wake umezingatia uchambuzi wa data kitaamuli. Matokeo ya makala hii yanatokana na utafiti wa maktabani na uwandani uliofanyika Zanzibar kuanzia mwezi Machi hadi Aprili 2026. Utafiti wa maktabani umefanyika kupitia udurusu wa maandiko mbalimbali pamoja na usikilizaji wa video zilizohifadhiwa *ZBC* na *YouTube*. Aidha, data za uwandani zimekusanywa katika maeneo yaliyomo katika Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar. Tulitumia mbinu ya usampulishaji tajwa

kuwapata watoataarifa 40 waliohusishwa katika utafiti huu. Mbinu hii ilitusahilishia kuwapata watoataarifa tuliowataka kwa lengo la kujibu maswali ya utafiti. Pia, data za uwandani zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usaili na hojaji, mbinu hizo ziliwahusisha wale waliokusudiwa kwa minajili ya kutoa taarifa zilizohitajika katika utafiti huu.

Katika kuhakikisha uaminifu wa data, watoataarifa walichaguliwa kutoka makundi tofauti ya kijamii ikiwamo wazee walioshuhudia moja kwa moja utekelezaji wa sera na mipango ya Rais Karume, walimu wastaafu waliofundisha kipindi hicho, na watunza kumbukumbu wa taasisi kama Nyaraka za Taifa Zanzibar. Mbinu ya usaili ilitoa nafasi ya kupata maelezo ya kina yasiyopatikana kwenye maandiko, ilhali hojaji iliwezesha kukusanya taarifa za jumla kutoka kwa watoataarifa wengi kwa muda mfupi. Data zilizokusanywa kupitia mbinu hizo kwa pamoja zilifanikisha kufikia lengo mahususi la makala hii, yaani kubainisha na kuchambua sera, matamko na mipango ya Kiswahili iliyowekwa na Rais Karume.

4.0 Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Kama ilivyodokezwa hapo awali (taz. §1.0), makala hii inahusu mchango wa Rais Abeid Aman Karume katika kuweka msingi wa maendeleo ya Kiswahili Zanzibar. Sehemu hii inawasilisha matokeo kwa kufuata mpangilio wa sera, matamko na mipango ya Kiswahili iliyowekwa na serikali yake, ambapo kila sera au tamko linawasilishwa kama data, likifuatiwa na uchambuzi unaolihusisha moja kwa moja na mihimili ya nadharia iliyotumika. Kama itakavyoonekana, sehemu hizi tatu hazipaswi kuonekana kama vipengele huru visivyohusiana, bali kama pande tatu za mchango mmoja mzima wa kiongozi mmoja aliyeamua kuweka Kiswahili katikati ya mradi wake wa kitaifa.

4.1 Sera za Kiswahili chini ya Utawala wa Rais Karume

a) Sera ya Kiswahili kuwa Lugha Rasmi Serikalini

Miongoni mwa sera bayana zilizowekwa na Rais Abeid Amani Karume ni uamuzi wa kuifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya shughuli zote za kiserikali, ukibadilisha sera ya kikoloni iliyokipa Kiingereza hadhi hiyo. Kabla ya Mapinduzi, kama ilivyoelezwa katika §1.0, lugha ya Kiswahili haikupewa nafasi ya kutumiwa kama lugha rasmi serikalini; Kiingereza ndicho kilichokuwa na hadhi hiyo. Mara tu baada ya Mapinduzi, sera hii ilibadilishwa kabisa, kama linavyoeleza gazeti la Kweupe (1964):

> *Mheshimiwa rais kwa nasaha za Baraza la Mawaziri na Halmashauri ya Upinduzi, amefurahishwa na kukata shauri kwamba, lugha ya Kiswahili itakuwa lugha ya serikali ya nchi yetu. Serikali ya Jamhuri ya Unguja na Pemba, imefuta sheria ya serikali ya zamani iliyopinduliwa iliyofanya Kiingereza kuwa lugha ya serikali. Kwa hivyo, serikali ya Jamhuri ya Unguja na Pemba, inatamka kuwa mfanyakazi wa serikali ajifundishe Kiswahili na kukijua kwa mifano kama inavyoyumkinika.*
>
> Chanzo: Kweupe (1964:4).

Dondoo hilo linaonesha dhahiri kwamba Rais Abeid Aman Karume aliweka msingi na juhudi za makusudi katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili kwa kutunga sera bayana, si kwa bahati au shinikizo la nje, bali kwa uamuzi wa ndani wa serikali yake mwenyewe. Kauli hiyo aliitoa Rais Karume katika mkutano wa hadhara uliofanyika siku ya Jumapili, tarehe 24 Oktoba 1964, ambapo gazeti la Kweupe lilibeba kichwa cha habari kilichosomeka "Mambo yote kwa Kiswahili maofisini". Akisisitiza sera hiyo, Rais Karume alieleza kuwa kwa kuwa serikali ni ya Waafrika, ni lazima itumike lugha ya Waafrika, na aliwataka wananchi kutumia Kiswahili

wanapokuwa ofisini na mikataba yote iandikwe kwa Kiswahili, kama alivyosema:

> *Madhali serikali ya Waafrika itumike lugha ya Waafrika ilipokuwa ikitumika lugha ya kigeni, tukenda mgongomgo, leo lazima twende usoni kwa sababu ni mali yetu... Wenyewe wananchi muingie katika maofisi muendeshe serikali yenu, muanzishe katika maofisi lugha ya Kiswahili. Mtu akipata cheti cha serikali au mkataba wa mauziano na mwenzake uandikwe kwa lugha yake... Aseme hii ni karatasi madhubuti baina yako na huyu, hii itamuwezesha mwanawananchi wa darasa la sita kuendesha serikali yake.*
>
> Chanzo: Kweupe, (1964:582).

Kuanzia Novemba 1964, sera hii ilianza kutekelezwa rasmi maofisini, na Rais Karume aliendelea kufafanua umuhimu wake kwa kufichua jinsi wakoloni walivyodanganya kwamba Kiswahili hakiwezi kutumika katika mambo rasmi. Ushahidi huu unasadifu vyema mhimili wa kwanza wa nadharia iliyoongoza utafiti huu, yaani mipango ya hadhi ya lugha: Rais Karume, akiwa kiongozi mwenye mamlaka, alipangilia moja kwa moja matumizi ya Kiswahili kwa kukiondolea Kiingereza hadhi ya lugha ya serikali na kukipandisha Kiswahili katika nafasi hiyo. Kwa kufanya hivyo, sera hiyo haikubaki kwenye karatasi tu bali ilitekelezwa kwa vitendo maofisini kote Unguja na Pemba, hatua iliyoonesha uzito wa mchango wa Rais Karume binafsi katika kuipa Kiswahili mamlaka ya kisheria isiyokuwepo hapo awali.

b) Sera ya Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia na Elimu Bure

Sera nyingine bayana iliyowekwa na Rais Karume ilihusu elimu. Mnamo tarehe 1 Aprili 1964, Rais Abeid Karume alitangaza skuli zote za kikabila kuwa mali ya serikali, na ilipofika tarehe 23 Septemba 1964, alitangaza sera ya elimu bure kama

linavyoeleza gazeti la Kweupe (1964):

> *Lifuatatalo ni tangazo la kuendeleza mbele elimu lililotolewa na Mheshimiwa Makamo wa Rais wa kwanza katika mkutano na waandishi wa magazeti mnamo tarehe 23 Septemba, 1964... Sasa tunawapa habari wananchi wote kuanzia leo wajue kwamba fees (malipo) ya skuli zote za Unguja na Pemba zimeondoka. Wananchi wote watapata elimu ya bure bila malipo.*
>
> Chanzo: Kweupe, (1964:417).

Sanjari na sera ya elimu bure, serikali ya Rais Karume ilibadili sera ya lugha ya kufundishia kwa kukifanya Kiswahili kuchukua nafasi ya Kiingereza kuanzia darasa la 1 hadi la 7. Tibategeza na du Plessis (2018) wanaeleza kwamba mwaka 1967 ndio mwaka ambao Kiswahili kilichukua rasmi nafasi ya Kiingereza katika elimu ya msingi, hadi kuzungumza Kiingereza hadharani kukemewa. Sera hii ilihusisha pia elimu ya sekondari, ambapo Kiswahili kilifanywa somo la lazima kwa sheria, mwanafunzi asiyefaulu Kiswahili katika kidato cha 4 hakupewa cheti hata kama amefaulu masomo mengine yote, na vipindi vya Kiswahili viliongezwa hadi kufikia 6 hadi 8 kwa wiki, sawa na vipindi vya Kiingereza na Hisabati. Aidha, Kiingereza kilifutwa katika shughuli za shule nje ya darasa, na mwanafunzi aliyesikika akizungumza Kiingereza hadharani aliadhibiwa au alipewa kazi ya ziada, huku vitabu vya itikadi ya kisiasa vikitakiwa visomwe kwa Kiswahili katika kipindi maalumu cha siasa.

Sera hizi za elimu zinathibitisha mhimili wa mipango ya hadhi ya lugha, kwani ziliipandisha Kiswahili rasmi kutoka nafasi ya somo tu hadi kuwa lugha kuu ya mfumo mzima wa elimu. Uamuzi huu wa Rais Karume ulikuwa na maana kubwa zaidi ya kiisimu: kwa kuunganisha elimu bure na lugha ya taifa katika tangazo moja, alihakikisha kwamba kizazi kizima kilichokuwa kikijengwa baada ya

Mapinduzi kingekulia kikijua na kuthamini Kiswahili kama lugha ya elimu na maendeleo, jambo lililoweka msingi thabiti kwa vizazi vijavyo.

c) Sera ya Matumizi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari

Rais Karume aliweka pia sera bayana kuhusu lugha ya vyombo vya habari. Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) ilielekezwa kutangaza asilimia 98 ya vipindi vyake kwa Kiswahili sanifu, hatua iliyogeuza redio kuwa darasa la umma (Khamis, 1974). Akizungumza na wanahabari tarehe 8 Mei 1970 kupitia Kweupe, Rais Karume alisisitiza umuhimu wa uaminifu na matumizi sahihi ya lugha katika habari:

> *Redio chombo muhimu ni mdomo wa taifa. Redio za Tanzania lazima zitangaze habari za kweli... Idara ya Habari na Utangazaji, ni Idara muhimu sana katika nchi kwani ndiyo mdomo wa taifa. Kwa hivyo kazi zake lazima zitekelezwe kwa uaminifu na uangalifu mkubwa ili kuweza kueleza habari za kweli.*
>
> Chanzo: Kweupe, (1970:1).

Sera hii ilihitaji waandishi wa habari kutumia Kiswahili sanifu kinachoeleweka kwa wananchi, na kuwataka wakuu wa uandishi kuzipitia habari kwa uangalifu kabla ya kuzitoa. Kwa mtazamo wa nadharia iliyotumika, sera hii nayo ni sehemu ya mipango ya hadhi ya lugha, kwa kuwa iliweka wazi nafasi ya Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano ya umma kupitia chombo chenye ushawishi mkubwa kama redio na magazeti. Sera hii ilisaidia kuondoa kwa kiasi kikubwa matumizi ya Kiingereza na Kiarabu kwa umma, na kuufanya Kiswahili kuwa lugha pekee inayounganisha wananchi wa matabaka na maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba.

4.2 Matamko ya Kiswahili kama Alama ya Utaifa na Uzalendo

Mbali na sera, utafiti umebaini kuwa Rais Abeid Karume alitoa matamko kadhaa ya hadharani yaliyokigeuza Kiswahili kutoka lugha ya mawasiliano hadi alama ya utaifa. Tarehe 13 Januari 1964, siku moja tu baada ya Mapinduzi, kabla hata ya kusubiri Muungano, Rais Karume alitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa sambamba na lugha rasmi, akisema:

> *Kuanzia leo lugha ya utawala, mahakamani na bunge itakuwa ni Kiswahili. Kiingereza kimekwisha, kiongozi asiyejua Kiswahili, hafai kutuongoza.*
>
> Chanzo: Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, (1965:5).

Tamko hili halikubaki kwenye maneno tu, bali lilitekelezwa kwa vitendo: tarehe 12 Januari 1965 Rais Karume alipiga marufuku mawaziri wote kutumia Kiingereza (Mbughuni, 1974). Kauli hiyo ya Rais Abeid Karume ni ushahidi tosha kwamba alitumia hotuba zake kama chombo kikuu cha kugeuza Kiswahili kutoka lugha ya mawasiliano hadi alama ya utaifa na kipimo cha uzalendo. Katika matamko mengine, aliunganisha uhai wa nchi na lugha kwa kutamka: "Kiswahili ni damu ya taifa. Tulipopigania uhuru, tulipiga kelele kwa Kiswahili. Sasa kimekomaa kiwe lugha ya utawala na kazi" (Mbughuni 1974:147). Kauli hii iliwafanya wananchi waone kuwa kukipenda Kiswahili ni sawa na kuipenda Zanzibar na kukikana ni kuhatarisha nchi. Aliweka pia Kiswahili kuwa sharti la utambulisho wa kitaifa: "Kuanzia leo kiongozi asiyejua Kiswahili hafai kutuongoza kwa kuwa ni kibaraka wa mkoloni" (Karume 1965 kama alivyonukuliwa na Mbughuni 1974:23), akitengeneza utambulisho mpya kwamba Mzanzibari halisi ni msemaji wa Kiswahili, na Kiingereza kikawa alama ya ukoloni. Aidha, alifuta tofauti za kikabila kwa tamko lililosema: "Mmakunduchi, Mshirazi, Mngazija, Mtumbatu sote tunaunganishwa na Kiswahili. Kikifa na Zanzibar imekufa. Tusipokienzi tutatawaliwa tena" (Karume, 1968 kama alivyonukuliwa na Mbughuni 1974:187).

Kwa njia hiyo, hotuba za Karume zikawa darasa la taifa ambapo Kiswahili kilifundishwa kama hisia ya umoja badala ya somo la darasani pekee.

Tamko jingine la kihistoria lilitolewa tarehe 12 Februari 1965, wakati wa sherehe ya mwaka mmoja wa Mapinduzi, mbele ya mabalozi kutoka nchi tisa, ambapo Rais Karume alikataa kutumia Kiingereza mbele ya wageni:

> *Waheshimiwa mliohudhuria leo hapa, tutatoa hotuba yetu kwa lugha ya Kiswahili lakini halafu itapatikana tafsiri kwa ufupi kwa lugha ya Kiingereza. Na halafu leo leo wajumbe wote wa nchi mbalimbali watapata kopi ya hotuba hiyo. Hatutaacha lugha yetu kwa sababu kuna mgeni hapa.*
>
> Chanzo: Kweupe (1965:1).

Kitendo hicho cha kijasiri kilichofanywa na Rais Abeid Karume kilipindua utamaduni wa kikoloni uliokuwa ukitaka viongozi wa Kiafrika wahutubie kwa Kiingereza. Kwa Wazanzibari, hatua hiyo ilijenga utaifa kwa kuthibitisha kuwa Mapinduzi na sherehe yake ni mali yao na kwa lugha yao. Dunia nayo ilijenga uzalendo kwa kutuma ujumbe kuwa taifa huru halidondoshi lugha yake ili kumuelewesha mgeni. Tamko jingine muhimu lilitolewa tarehe 9 Disemba 1964 Mnazi Mmoja, wakati Rais Karume alipotangaza kubadilishwa kwa jina la Uwanja wa King George kuwa Uwanja wa Amani, akisema kuwa amani ndiyo msingi wa Mapinduzi (Kweupe, 1964:1). Kwa mtazamo wa Nadharia ya Sera na Mipango ya Lugha, matamko haya yanawakilisha jinsi mipango ya hadhi ya lugha ilivyotangazwa hadharani na kuenezwa kwa jamii kupitia lugha ya kihisia na kiuzalendo: Rais Karume hakuridhika na kutunga sera peke yake, bali alitumia hotuba na matamko kama chombo cha kujenga utaifa na kufuta kumbukumbu za kikoloni akilini mwa wananchi. Matamko haya ndiyo kiungo kilichounganisha sera zake (za kikaratasi) na mipango yake (ya kivitendo), kwa kuwapa wananchi sababu

za kihisia za kushiriki katika mchakato mzima wa maendeleo ya Kiswahili.

4.3 Mipango ya Kiswahili: Utekelezaji na Ukuzaji wa Lugha

a) Mpango wa Kuunda Istilahi Mpya

Katika kutekeleza sera na matamko yake, Rais Karume aliweka mpango madhubuti wa kuiendeleza lugha ya Kiswahili kimuundo. Kazi iliyobaki, kwa mujibu wake, ilikuwa ni kuzidi kuitukuza lugha ya taifa. Aliwasihi watunzi wa mashairi na waandishi wengine wazidishe juhudi za kuiendeleza, kuitilia nguvu na kuiongezea utamu lugha ya Kiswahili, na iliundwa Halmashauri chini ya Wizara ya Elimu na Mila iliyopewa jukumu la kutengeneza maneno mapya ya Kiswahili kila panapohitajika kutokana na uvumbuzi wa mambo mapya. Jambo hili lilionekana kuwa la lazima kwa kuwa kila siku huvumbuliwa mambo mapya, na kwa hivyo iliwalazimu Wazanzibari kuunda maneno mapya ili lugha yao ikue na iendelee kuwafaa katika mambo yao yote. Mpango huu unaakisi moja kwa moja mhimili wa pili wa nadharia iliyotumika, yaani mipango ya mwili wa lugha, ambao unahakikisha kwamba lugha iliyoteuliwa inakuzwa kimsamiati ili isibaki tuli.

b) Mpango wa Kubadilisha Majina kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili

Kufuatia tamko la Mnazi Mmoja, Rais Karume alisimamia mpango kamili wa kubadilisha majina ya maeneo, skuli, barabara, hospitali na viwanja kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili, akiamini kwamba kubadilisha jina ni kubadilisha fikra. Hii ilikuwa sehemu ya Mapinduzi ya Kiutamaduni, kwani kila neno jipya lilitangazwa na Karume mwenyewe kwenye mkutano wa hadhara Mnazi Mmoja, kisha likatangazwa na vipazasauti na kuchapishwa kwenye Kweupe, mbinu iliyowarahisishia wananchi kulisikia na kulijua siku hiyohiyo. Katika utekelezaji wake, majina ya wafalme wa Kiingereza kama King George, Queen Victoria na

Prince of Wales yaliondolewa na badala yake yakatumika majina ya Kiswahili ya Mapinduzi, Lumumba, Amani na Uhuru. Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mila, Ali Sultan Issa, tarehe 16 Januari 1965 alitangaza majina mapya ya Kiswahili kwa skuli kumi: St. Joseph's Convent ikawa Mtakuja Skuli, St. Monica's School ikawa Mkunazini Skuli, St. Paul's School ikawa Kiungani Skuli, Datu Hemani School ikawa Ukutani Skuli, Hindi Sunni Madrassa School ikawa Kajificheni Skuli, Madrassa-el-Mohammedieh School ikawa Hamamni Skuli, Hindoo Free Girls' School ikawa Forodha Mchanga Skuli, Holmwood School ikawa Kidongo Chekundu Skuli, Town Primary Girls' School ikawa Forodhani Skuli, na Aga Khan School ikawa Kidutani Skuli (Kweupe, 1965:53).

Zoezi hili la kubadilisha majina lilipokelewa na kutekelezwa kwa mikono miwili na mawaziri, viongozi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla, na kuleta matumaini mapya kwa wananchi wa Zanzibar. Matokeo yake yaliweka msingi imara wa kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili, lakini pia kufutwa kwa kumbukumbu za kikoloni na kuimarishwa kwa utambulisho wa kitaifa. Hivyo, kubadilisha majina hakikuwa kitendo cha kiisimu tu, bali kilikuwa kitendo cha kisiasa cha kubadilisha fikra ya taifa. Mpango huu wa kimfumo unaonesha jinsi tamko la kisiasa lilivyotafsiriwa kuwa mpango halisi wa mwili wa lugha uliogusa maisha ya kila siku ya wananchi, kuanzia jina la skuli anayosoma mtoto hadi jina la uwanja anaocheza.

c) Mpango wa Mitihani ya Walimu

Ili kuhakikisha ubora wa Kiswahili sanifu shuleni, Rais Karume aliweka mpango wa kuwapima walimu kwa mtihani kabla ya kupandishwa daraja, mfumo uliofanya kazi kuanzia 1965 hadi 1972. Mtihani huo ulitungwa kwa Kiswahili sanifu na ulihusisha maswali ya kuandika insha, sarufi na msamiati, pamoja na maswali ya

itikadi ya siasa, Azimio la Arusha, Ujamaa, hotuba za Rais Abeid Karume na mbinu za kufundisha Kiswahili. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (1964-1967) inaeleza:

> *Baada ya mapinduzi serikali ya Karume ilianzisha mitihani ya lazima kwa walimu. Kupandishwa daraja, kulitegemea kufaulu mitihani ya Kiswahili na itikadi ya kisiasa na walimu walioshindwa hawakupandishwa.*
>
> Chanzo: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, (1964-1967:42-58).

Kila baada ya miaka miwili hadi mitatu, mwalimu alilazimika kufanya mtihani huo ili apande daraja; aliyeshindwa hakupandishwa, mshahara wake ulibaki palepale, na alitakiwa kurudia mtihani baada ya miezi sita. Mwalimu aliyeshindwa mara mbili hadi tatu mfululizo alipelekwa mafunzo ya kisiasa au kufukuzwa kazi. Sababu za msingi za mpango huu, kwa mujibu wa mtoataarifa mmoja, zilikuwa kuondoa walimu wakoloni wasiojua Kiswahili sanifu, kuhakikisha ujamaa unafundishwa kwa Kiswahili, na kupunguza gharama za kuajiri walimu wapya kwa kuwapima na kuwapandisha wale waliopo. Mpango huu uliwasaidia hasa walimu waliosoma baada ya 1964, na hatimaye Kiswahili cha shuleni kikawa sanifu zaidi kwa sababu mwalimu asiyejua sarufi hakuweza kupandishwa. Mpango huu unadhihirisha mhimili wa upataji lugha, kwa kuwa ulihakikisha kwamba wale wanaofundisha lugha wanaimudu wenyewe kwa kiwango cha juu, jambo lililokuwa na athari ya moja kwa moja kwa ubora wa Kiswahili kilichofundishwa kwa vizazi vilivyofuata.

d) Mpango wa Kufuta Ujinga (Elimu ya Watu Wazima)

Mpango mkubwa zaidi wa upataji lugha uliosimamiwa na Rais Karume ulikuwa kampeni ya kufuta ujinga, iliyoanzishwa mwishoni mwa mwaka 1964 hadi 1970, kwa lengo la kila Mzanzibari kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa Kiswahili

ifikapo mwaka 1975, chini ya kauli mbiu "usome leo upate kesho" iliyoandikwa kila kijiji. Kila shehia ililazimika kufungua darasa la jioni mahali popote iwe msikitini, ofisini, skuli au chini ya mti, na wanafunzi wa sekondari pamoja na walimu walifundisha watu wazima bila malipo. Kampeni hii ilikuwa ya lazima, na aliyekosa kuhudhuria alitozwa faini ya shilingi 20. Iliundwa Halmashauri ya Kueneza Elimu (HKE) iliyosimamia mpango huo, kama linavyoeleza Kweupe (1965):

> *Bwana Ali Hassan ambaye alikuwa katibu mkuu wa wizara ya Elimu na Mila, alitunga kitabu maalumu juu ya kufundisha watu kusoma na kuandika Kiswahili, na halmashauri hii (HKE) imetengeneza mpango maalumu wa kusomesha kwa kufuata mabuku hayo.*
>
> Chanzo: Kweupe, (1965:166).

Redio na magazeti pia vilitumika kikamilifu katika mpango huu: kila siku saa 12:30 jioni kulikuwa na kipindi kiitwacho somo la watu wazima ambapo watu wazima walifundishwa herufi hewani, na gazeti la Kweupe lilikuwa na ukurasa maalumu uliosema Jifunze Kusoma, uliosheheni hadithi nyepesi na mazoezi mbalimbali. Ndani ya miezi sita tu, wananchi elfu thelathini na tano (35,000) walikuwa wameanza kusoma na kuandika huko Pemba, na wanawake na wanaume elfu hamsini na sita (56,000) walikuwa wakipata mafunzo hayo visiwani kote. Tarehe 12 Machi 1965, Rais Karume alikabidhi vyeti kwa wazee 650 waliohitimu mafunzo hayo:

> *Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Abeid Amani Karume siku ya Ijumaa tarehe 12 Machi, 1965, alitoa shahada mia sita na khamsini (650) kuwapa akina mama na akina baba waliopasi katika mafunzo ya kusoma na kuandika. Sherehe hiyo iliyofanywa huko katika Bustani ya Manispaa, ilihudhuriwa na waziri wa Elimu na*

> *Mila, Mheshimiwa Ali Sultan Issa pamoja na baadhi ya mawaziri wengine. Memba wa Baraza la Mapinduzi, Makonseli wa nchi za nje na wananchi wengi.*
>
> Chanzo: Kweupe, (1965:130).

Kufikia mwaka 1972, asilimia 75 ya watu wazima Zanzibar walijua kusoma na kuandika Kiswahili, kutoka asilimia 23 mwaka 1964, hali iliyoipatia Zanzibar sifa ya kuwa nchi ya kwanza Afrika kufuta ujinga wa kusoma na kuandika kwa kiwango kikubwa. Ilipofika mwaka 1973, UNESCO ikaipongeza Zanzibar kwa kuwa mfano wa kuigwa, pongezi zilizotokana moja kwa moja na kampeni ya Rais Abeid Karume (Bakari, 2001). Mpango huu wa kufuta ujinga unaonesha kwa uwazi kabisa mhimili wa upataji lugha uliotawala nadharia ya utafiti huu: Rais Karume, kama kiongozi mwenye mamlaka, alihakikisha jamii yake inapata fursa halisi ya kujifunza Kiswahili kupitia mitaala isiyo rasmi, vyombo vya habari na mafunzo ya watu wazima, jambo lililobadilisha kabisa uwiano wa watu wanaojua kusoma na kuandika ndani ya kipindi kifupi cha miaka minane pekee ya uongozi wake.

4.4 Muhtasari wa Mchango wa Rais Karume katika Maendeleo ya Kiswahili

Sehemu zilizotangulia zimeonesha kwamba mchango wa Rais Abeid Amani Karume katika maendeleo ya Kiswahili Zanzibar haukuwa tukio moja au uamuzi mmoja, bali ulikuwa mfumo mzima wa sera, matamko na mipango iliyofungamana na kutegemeana. Jedwali lifuatalo linatoa muhtasari wa mchango huo kwa kuonesha uhusiano kati ya kila kipengele na mhimili wa nadharia uliokitawala, pamoja na matokeo yake makuu.

Kipengele	Mifano Muhimu	Mhimili wa Nadharia	Matokeo Makuu
Sera	Kiswahili lugha rasmi serikalini; Kiswahili lugha ya kufundishia; sera ya vyombo vya habari (98% STZ)	Mipango ya Hadhi ya Lugha	Kiswahili kupata mamlaka rasmi ya kisheria katika ofisi, mahakama na elimu
Matamko	Tamko la Taifa la 13 Januari 1964; tamko kwa mabalozi 9; tamko la kuunganisha makabila; tamko la Mnazi Mmoja	Uenezaji wa Hadhi kwa Jamii (kwa lugha ya kihisia/kiuzalendo)	Kiswahili kuwa alama ya utaifa, umoja na uzalendo miongoni mwa wananchi
Mipango	Halmashauri ya istilahi mpya; ubadilishaji wa majina; mitihani ya walimu; kampeni ya kufuta ujinga	Mipango ya Kongoo ya Lugha na Upataji Lugha	Kiswahili kukua kimsamiati, ubora wa ufundishaji kuongezeka, na asilimia 75 ya watu wazima kujua kusoma na kuandika kufikia 1972

Kama jedwali hilo linavyoonesha, sera ziliweka msingi wa kisheria, matamko yaliupa msingi huo maana ya kihisia na kiuzalendo iliyofanya wananchi wauunge mkono kwa moyo, na mipango ndiyo iliyogeuza sera na matamko hayo kuwa uhalisia wa kila siku maishani mwa Wazanzibari. Ni mwingiliano huu wa vipengele vitatu ndio unaoelezea kwa nini, tofauti na nchi nyingine nyingi za Afrika zilizopata uhuru kipindi kama hicho, Zanzibar chini ya Rais Karume iliweza kubadili kabisa lugha ya utawala wake ndani ya muda mfupi bila upinzani mkubwa wa kijamii. Mchango wa Rais Karume, kwa hiyo, hauwezi kueleweka vizuri kwa kuangalia sera, matamko au mipango kwa kujitegemea; ni lazima vionekane kama sehemu za mradi mmoja mzima wa kisiasa wa kuifanya Kiswahili kuwa msingi wa taifa jipya la Zanzibar.

5.0 Mapendekezo na Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa kuchambua mchango wa Rais Abeid Aman Karume katika kuweka msingi wa maendeleo ya Kiswahili Zanzibar, kwa kutenganisha bayana sera, matamko na mipango aliyoiweka. Uchunguzi umebaini kuwa, kwa upande wa sera, Karume alitangaza Kiswahili kuwa lugha rasmi serikalini, lugha ya kufundishia elimu, na lugha kuu ya vyombo vya habari. Kwa upande wa matamko, alitumia hotuba zake kukigeuza Kiswahili kutoka lugha ya mawasiliano hadi alama ya utaifa, umoja na uzalendo. Aidha kwa upande wa mipango, alisimamia utekelezaji thabiti kupitia kampeni ya kufuta ujinga, mitihani ya walimu, uundaji wa istilahi mpya, na ubadilishaji wa majina ya maeneo. Kwa pamoja, sera, matamko na mipango hiyo iliweka msingi thabiti wa kukiendeleza Kiswahili kama lugha ya taifa na chombo cha umoja Zanzibar, ikithibitisha mihimili yote mitatu ya Nadharia ya Sera na Mipango ya Lugha iliyoongoza utafiti huu.

Kwa msingi huo, tunapendekeza yafuatayo: kwanza, viongozi wa sasa waendelee kukuza misingi iliyowekwa na Rais Karume, kwa kutunga sera bayana za lugha na kuzitekeleza kwa vitendo, si kwa matamko peke yake. Pili, kufanyike tathmini ya kina ya athari za sera na mipango hiyo kwa vizazi vya sasa vya Zanzibar, ili kubaini kama misingi hiyo bado inatekelezwa au imepungua nguvu kwa wakati. Tatu, kufanyike utafiti linganishi kati ya msingi uliojengwa na Rais Karume wa Zanzibar na ule uliojengwa na Rais Nyerere wa Tanzania Bara katika upangaji wa lugha ya Kiswahili, ili kubaini mafanikio na changamoto za kila upande. Nne, taasisi za elimu na utafiti kama Chuo cha Taifa cha Utalii na vyuo vikuu vya Zanzibar na Tanzania Bara zihamasishwe kuandaa kumbukumbu na machapisho zaidi kuhusu michango ya viongozi waasisi wa Kiswahili, ili historia hii isipotee kwa vizazi vijavyo.

Mwisho, mchango huu wa Rais Sheikh Abeid Amani Karume ni ishara tosha ya utashi wa kisiasa katika kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Kupitia sera alizotunga, matamko aliyoyatoa na mipango aliyoisimamia, Rais Karume aliweka msingi ambao umekuwa daraja la maendeleo ya Kiswahili hadi hivi leo, na unastahili kuenziwa na vizazi vyote vinavyofuata kama sehemu ya urithi mkubwa wa taifa la Zanzibar.

Changamoto na Upungufu ya Utafiti

Kama ilivyo kwa tafiti nyingine za kihistoria, utafiti huu ulikabiliwa na changamoto kadhaa zinazostahili kutajwa. Kwanza, baadhi ya nyaraka za kihistoria za kipindi cha 1964-1972, hususan baadhi ya matoleo ya gazeti la Kweupe na kumbukumbu za mikutano ya Baraza la Mapinduzi, zimehifadhiwa kwa hali isiyo nzuri katika Nyaraka za Taifa Zanzibar, jambo lililoathiri kwa kiasi upatikanaji wa data fulani za kina zaidi. Pili, watoataarifa wengi waliohusika moja kwa moja na utekelezaji wa sera na mipango ya kipindi hicho tayari wamefariki au wamezeeka sana, hivyo

kumbukumbu zao huenda zisiwe sahihi kikamilifu kwa asilimia mia moja, ingawa jitihada zilifanyika kuzihakiki dhidi ya nyaraka za maandishi pale ilipowezekana. Tatu, kwa kuwa Rais Karume mwenyewe hakuandika kumbukumbu (memoir) rasmi, taarifa nyingi kumhusu zinategemea magazeti ya wakati huo na maandiko ya wasomi waliokuja baadaye, jambo linaloweza kubeba mtazamo wa waandishi hao. Pamoja na changamoto hizo, tahadhari kubwa ilichukuliwa kuhakikisha kuwa kila dai kuu limeungwa mkono na vyanzo zaidi ya kimoja, iwe cha maandishi au cha mdomo, ili kuongeza uaminifu wa matokeo yaliyowasilishwa. Hivyo, tafiti zijazo zinashauriwa kutafuta na kuhifadhi kidijiti nyaraka zilizosalia za kipindi hiki kabla hazijapotea kabisa.

Marejeo

Bakari, M. A. (2001). *The Democratisation Process in Zanzibar: A Retarded Transition*. Hamburg: Institute of African Affairs.

BAKIZA. (2020). *Dk. Shein na Maendeleo ya Kiswahili Zanzibar 2010-2020.* Zanzibar: BAKIZA.

Haugen, E. (1966). *Language Conflict and Language Planning: The Case of Modern Norwegian*. Cambridge: Harvard University Press.

Khamis, S. (1974). Sauti ya Tanzania Zanzibar na Maendeleo ya Kiswahili. Zanzibar.

Kweupe. (1964, Septemba 24). Toleo la 109. Nyaraka za Taifa Zanzibar: MW8/1.

Kweupe. (1965, Machi 16). Toleo la 31. Nyaraka za Taifa Zanzibar: MW8/1.

Kweupe. (1970, Mei 8). Toleo la 18. Nyaraka za Taifa Zanzibar: MW8/2.

Lofchie, M. F. (1965). *Zanzibar Background to Revolution*. Princeton, NJ: Princeton University Press.

Mazrui, A. A. & Mazrui, A. M. (1995). *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mbughuni, L. A. (1974). *The Cultural Policy of the United Republic of Tanzania*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (1965). The Courts Decree. Zanzibar: Government Printer.

Shariff, A. (1991). *Zanzibar Under Colonial Rule.* London: James Currey Publishers.

Tibategeza, E. R. & du Plessis, T. (2018). The Prospects of Kiswahili as a Medium of Instruction in the Tanzanian Education and Training Policy. Journal of Language and Education, 4(1), 88-98.

The Citizen. (2025). Zanzibaris Mark 53rd Anniversary of Karume's Death with Calls for Unity and Development. Ilipatikana Aprili 18, 2026 kutoka thecitizen.co.tz.

Wizara ya Elimu Zanzibar. (1988). Sera ya Elimu. Zanzibar: WE.